

KUFANYWA WANA WENYE MAMLAKA KIROHO



Asante, Ndugu Neville. Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha sana kuwa hapa asubuhi ya leo, na kupata utangulizi huu kutoka kwa mchungaji. Huo ulikuwa ni mzuri sana. Loo, unajua, nikizungumza juu ya farasi, unajua, walipofungwa hatamu, walijua kazi ilikuwa inakuja. Vema, ni, nina furaha sana Bwana hutufanya kuwa farasi wa kazi, ili tuweze kufanya kazi, bado. Kwa hivyo, kamwe, kamwe hatuchoki sana tusiweze kumtendea Bwana jambo fulani, endapo imetuangukia kulifanya. Ingawa, ni mchovu sana leo. Nilikuwa tu na wakati mgumu sana, katika siku chache zilizopita.

² Kwenda California, ilinibidi niende kwa kiberenge. Na, nakuambia, nena kuhusu kurushwa-rushwa! Kote huko nje, saa hamsini na tatu kufika huko, na kufika huko saa nane usiku. Saa kumi na moja, ilinibidi niamke na kwenda kuhubiri ibada ya redioni. Ndipo, Wafanyabiashara Wakristo, ilinibidi kuhubiri tena kwa ajili ya kusanyiko lao la kimataifa. Ndipo alasiri hiyo, nilihubiri kwenye maskani kubwa ya Kibaptisti, halafu. . . usiku huo. Na kisha tuliendelea tu, tukizungumza kila baada ya saa chache, mpaka hatimaye tukamalizia Jumatatu usiku kwenye Hekalu la Angelus. Ndipo tukapanda garimoshi saa tano, nayo ikachukua saa sitini na nne kufika nyumbani. Kwa hivyo unaweza kuwazia, niliingia, majuzi, na kuninii tu. . .

³ Na, jana, mke wangu alipokea simu hamsini na kitu, nije niwaombee watu. Jana asubuhi, pekee, mnaona, simu hamsini na kitu. Bila shaka, zote hazikuwa za huku. Zilikuwa—zilikuwa simu za kitaifa, lakini tu, “Je, unaweza kuja Florida? Unaweza kuja *huku*? Hii ni Louisville.” Wao. . . Utachagua je, kati ya hizo hamsini na tatu sasa, kwa asubuhi moja tu? Kwa hiyo, mwaweza kuwazia.

⁴ Kwa hiyo, jana alasiri, nilikuja kuona, miongoni mwa baadhi ya marafiki zetu wapendwa, jinsi ugonjwa wa ibilisi ulivyo. Kijana niliye kuwa namfahamu miaka mingi iliyopita, alionekana mzima sana, kama mwanariadha. Na sasa ni kama rika yangu, na angedhaniwa ana miaka tisini. Naye amelala, akifa huko Henryville. Rafiki wa ndugu yangu mwema hapa, Ndugu Neville, alikuwa Kermit Spurgeon; baba yake, mhubiri wa Injili, na mwalimu wa shule, na mtu mzuri sana.

⁵ Niliingia humo nyumbani baada ya Ndugu Neville kuniambia mvulana huyo alikuwa yuafa, nasi tulikuwa na majaliwa makuu ya kumwongoza kwa Bwana Yesu, jana, kwa

ajili ya wokovu wa nafsi yake. Nami pamoja na mke wake tumekubaliana na kumwombea kwa uaminifu, baada ya kuliwa na kansa; kutoka pauni mia mbili na kitu, kushuka hadi, nina shaka kama ana uzito wa sitini. Kwa hiyo, tunaamini na kushikilia, ya kwamba Mungu atamponya. Kwamba, hatujui kitakachotokea. Lakini, jambo moja tujualo, ni kwamba amepita toka mautini kuingia Uzimani. Nami nawazia yale maskini baba yake kipofu aliwazia wakati huo ujumbe ulipomjia, baada ya hiyo miaka yote ya kumwombea, na hata hivyo. “Mlee mtoto katika njia impasayo,” mnaona. Nami najua alikuwa na mfano sahihi mbele yake.

⁶ Tukaondoka huko, tukashuka kuingia New Albany, kwa Bibi Slaughter aliyeishi huku nje, nao madaktari walikuwa wamempa hadi saa kumi na mbili, kuishi. Kwa hiyo, ilikuwa ya kusikitisha sana sana, katika kungoja. Na mahali tofauti.

⁷ Kijana mmoja alikuwa akiishi jirani yangu pale, yeye anatembea tu, kijana wa kawaida, akifanya kazi kwa Kampuni ya Simu ya Bell, yapata umri wa miaka ishirini na kitu. Alikuwa na. . . Baba wa watoto watatu au wanne. Msichana wake mdogo alianguka hivi majuzi na kuvunja mkono wake. Akaanza kupata hisia ya ganzi mkononi mwake; ikampoozesha. Hata hawajui ana shida gani. Amelala kule, naye huyo hapo.

⁸ Jambo moja tu baada ya lingine, na ugonjwa pande zote. Nina furaha sana kuwa kuna njia ya kuepukia. Nina furaha sana kwamba haitubidi kukaa hapa milele, pia, sivyo? Je, tungefanya nini kama ingenilazimu kuishi katika nyumba hii ya wadudu milele? Nina furaha sana kwamba kuna mlango uliofunguliwa. Na hivyo ndivyo tu dunia ilivyo, ni nyumba tu ya wadudu. Ni. . . Mara tu unapofikiri kwamba tunaendelea vema, ndipo hili hapa jambo lingine linakuja, na, hata hivyo, hili hapa jambo lingine linakuja. Lakini, nina furaha sana kwamba kuna njia ya kuepukia; nina furaha sana kwamba Bwana Yesu amekuja na kuandaa njia kwa ajili yetu, njia ya kuepukia.

⁹ Kwa hiyo, asubuhi ya leo, Dada yangu mpendwa Cox alikuwa akiniambia kwamba mtu fulani anakuja, kwa kuwa tuliwaomba watu wa mahali hapo waje kuombewa, na labda wasingeweza kukaa ila kwa dakika chache tu. Na halafu labda ningewaombea kabla ya kuwa na ibada, na, halafu, kama iliwabidi kurudi.

¹⁰ Ndipo nikawazia, basi, kwa hao wengine waliotaka kubaki, kwa namna fulani ningeufupisha ujumbe wangu, asubuhi ya leo, kwa kuwa nimepwelewa na sauti, na—na inanibidi kwenda mara moja kwenye mkutano mwingine. Na kwa hiyo mimi. . . Nao mkutano wa Chicago unaanza Jumamosi ijayo.

¹¹ Na, halafu, nadhani ya kwamba saa imewadia ambapo sehemu hii ya nchi inapaswa kupokea kuzuriwa kukuu, kwa kuja kwa ndugu yetu muungwana, Billy Graham, huko Louisville, juma hili lijalo. Anaanza wakati uo huo, Louisville, ninaanza

Chicago. Kwa hivyo, nitarudi, hata hivyo, na—nataka kukutana naye, kibinafsi, wakati akiwa hapa. Na marafiki wengine watanitambulisha kwake. Nami nimekuwa moja kwa moja katika jiji lile lile, huko ng'ambo, na sehemu nyingi mbalimbali, lakini tu, kwa hiyo, hatukupata kukutana.

¹² Na—nami naliomba kanisa hili kwa uaminifu, na kundi hili la watu waliokusanyika hapa asubuhi ya leo, wauchukue mkutano huu moyoni mwao, kule Louisville.

¹³ Ninataka kusema hivi, kwa kupita tu. Je, ulijua kwamba asilimia themanini na saba ya vileo vyote hutoka Louisville, Kentucky, ambavyo—ambavyo vinanywewa Marekani? Themanini na saba. Je, unajua, yapata asilimia tisini ya tumbaku zote na kadhalika hutoka Louisville, Kentucky? Je, ulijua hicho ndicho kiti cha Shetani. Bila shaka ndicho. Bila shaka ndicho.

¹⁴ Mojawapo ya maeneo magumu sana yaliyopo ulimwenguni, ni eneo hili karibu na hapa, kupenya kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo. Ni wangapi wamepiga magoti wakilia, wakijaribu kuipenya nchi hii, Miji hii ya Falls, kwa ajili ya Bwana Yesu! Angalieni, Erickson, wale wote waliotoka, hata wakilia, jinsi walivyojaribu na kujaribu na kujaribu. John Sproul hata aliingia wazimu, kwenye Glory Barn kule, akijaribu awezavyo kukipenya hicho kitu kwa ajili ya Bwana Yesu. Jinsi wengine wamesimama jukwaani, katika Miji hii ya Falls, na kujaribu, wala hawakuweza kuipenya kwa ajili ya Bwana Yesu.

¹⁵ Sasa, nafikiri Billy Graham ni mmoja wa watu wanaojulikana sana ulimwenguni siku hizi, katika mambo ya kidini, nionavyo mimi. Bila shaka, tuna maaskofu na maaskofu wakuu. Lakini, nionavyo mimi, yeye ni mhubiri wa Injili, mtu wa Mungu. Na kwa hiyo—na kwa hiyo nafikiri yeye... Kama mashujaa wa Kikristo, pamoja, hebu tuungane na kuweka mioyo yetu pamoja, na kuuombea mkutano huo, kama vile hatujawahi kufanya hapo awali. Na tuombe kwamba Mungu, kwa namna moja ama nyingine, atatupa nafsi, na kukivunja kiti cha Shetani, ili wafunge kila kiwanda cha pombe na kuteketeza viwanda vya tumbaku, na kuyajaza makanisa na kuwa na kumwagwa halisi kwa Roho Mtakatifu kwa mtindo wa kale. Bwana abariki!

¹⁶ Sasa, nina jambo tofauti kidogo tu, lisilo la kawaida kwa kuanzia. Ndugu yangu ana mtoto hapa ambaye wanataka awekwe wakfu kwa Bwana. Nami nafikiri tutafanya hivyo kabla tu ya kuwaombea wagonjwa, Mungu akipenda. Na kama Dada Gertie atakuja kwenye piano. Na wale wote ambao wana watoto wadogo...

¹⁷ Sasa, katika Biblia, tunafundishwa hapa ya kwamba... Sasa, wengi—wengi, watu wengi, huita kuwabatiza, kuwanyunyizia maji, wanakuita ubatizo wa “watoto wachanga.” Vema, sasa, hiyo ni sawa. Naam. Haumdhuru mtoto mchanga, nami nina—nina hakika itakuwa sawa. Na, wengine, wana

njia zingine wanazofanya. Na, lakini, daima tunapenda, kwa karibu tu tuwezavyo, kukaa na njia ya Biblia ya kufanya jambo hilo. Na, njia ya Biblia ya kufanya jambo hilo, hakuna mahali katika Biblia walipowahi kufanya hivyo, na watoto wachanga. Ilikuwa. . .

Vema, sasa, wakati Agano la Kale, walitahiri.

¹⁸ Sijui kama wazee kadhaa watamsogeza huyu dada kidogo upande mmoja hapa, tafadhali, mpaka tutakapowaweka wakfu; dada aliye kwenye machela hapa. Na, kwa hivyo, hujali, dada mpendwa? Ni muda mfupi tu. Nasi. . .

¹⁹ Na kwa hiyo basi, katika Agano la Kale, wa—walimtahiri mtoto mchanga. Na katika. . . Walimtahiri mtoto mchanga.

²⁰ Na katika Agano Jipya, njia pekee waliyofanya, waliwaleta watoto wadogo kwa Bwana Yesu, Naye akawainua mikononi Mwake, akawabariki. Naye akasema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa maana walio kama hao Ufalme ni wao.”

²¹ Sasa kama kuna mama mwingine yeyote hapa, aliye na mtoto wao mchanga, ambaye wangependa kumweka wakfu kwa Bwana, tutafurahi kufanya hivyo wakati huu. Na sasa hebu sisi. . . kwa makini.

²² Sasa, jina la huyu jamaa mdogo ni nani? [Ndugu huyo anasema, “Robert Lynn.”—Mh.] Mvulana mdogo, Robert Lynn. Sasa, hiyo ni sawa kabisa. Sasa, huyu ni. . . naamini u—ulimwasili huyu mtoto mchanga. . . ? . . .

²³ Hii inaonyesha u—upendo wa mama kwa mtoto. Na tukiwazia jambo hili, wao wakiwa hawana watoto, walakini walitaka kumlea mmoja, wakamwasili mtoto huyu. Je, mnatambua kwamba sisi sote ni watoto wa kuasiliwa? Mungu alitupenda sana, hata akatufanya wana kwa Mwanawe, Kristo Yesu. Nasi sote ni watoto wa kuasiliwa. Basi, kumbukeni, kama baba na mama huyu anavyomfikiria huyu mtoto ambaye hakuwa na nyumba ya kwenda, wakampa makao, wapate kumlea na kumtunza. Hatukuwa na makazi ya kuendea, na Mungu akatupa makazi.

²⁴ Ni mtoto wa kuasiliwa. Jina lake ni Robert Lynn Branham; mtoto mzuri sana, mdogo.

Sasa na tuinamishe kichwa chetu.

²⁵ Baba yetu wa Mbinguni wa thamani, kama katika siku zilizopita, ni baba na mama wangapi waliowainua watoto wao wadogo wakawaweka mikononi Mwako! Nawe umesema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa maana walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.” Na huyu mtoto mdogo asiye na makazi, amepewa makazi, na Wewe umeweka mioyoni mwao upendo kwa mtoto huyu.

²⁶ Basi, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utambariki mama na baba huyu, wanapomlea huyu mtoto. Na alelewe katika nyumba ya maombi, na kufundishwa kwenda kanisani, na kumwishia Bwana Yesu. Mbariki, Baba mpendwa wa Mbinguni.

²⁷ Na, sasa, kama ungalikuwa hapa duniani, katika mwili wa kibinadamu kama tunaosimama asubuhi ya leo, wangemweka huyu mtoto mkononi Mwako. Lakini Wewe umeenda Mbinguni na ukatuagiza kuiendeleza hii huduma mpaka utakaporudi. Basi, Baba, kama vile ndugu yangu wa kuzaliwa anavyoweka mtoto mchanga mikononi mwangu, ninamkabidhi Kwako katika Jina la Kristo. Mbariki mtoto huyu na aishi na kuwa na afya njema na nguvu, na akue na kuwa mtumishi Wako. Wabariki baba na mama, nyumbani. Tunakupa Wewe, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

²⁸ Ubarikiwe, Agnes, uwe mama halisi; na wewe, Jesse, baba halisi kwa mtoto huyu. Na Mungu awabariki katika juhudi zenu. Na Mungu awe pamoja nanyi.

²⁹ U hali gani! Jina la mtoto ni nani? [Dada huyo anasema, “Robert Darrel.”—Mh.] Robert mwingine. Vema, hilo ni sawa. Robert Darrel.

³⁰ Na jina lako ni nani? [Dada huyo anasema, “Robertson.”—Mh.] Wewe ni kadogo. [“Naam.”] Na jina lako la mwisho? [“McCloud.”] McCloud. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

Tukileta miganda, tukileta miganda,
Loo, tutakuja kwa shangwe, tukileta miganda.

Kupanda asubuhi, kupanda usiku,
Kupanda adhuhuri na usiku wenye umande;
Baadaye mavuno, kisha wakati wa kuvuna,
Tutakuja kwa shangwe, tukileta miganda.

³¹ Naam, hiyo ni sawa. Kuleta miganda, hivyo ndivyo baba na mama hufanya: kuwaleta kwa Bwana Yesu.

³² Dada aliyelala juu ya machela, anaonekana kuwa mahututi kuliko wote, kadiri tuwezavyo kuona. Yuko kwenye machela. Na tungeninii. . . Ikiwa kuna mtu yeyote. . . Anataka kungoja kwa dakika chache tu, kuusikia Ujumbe, kabla ya kuombewa. Nami nafikiri hilo ni zuri sana, sana. Kama kuna mtu hapa ambaye hawezi kusubiri, na anataka kuondoka, na iwapo unataka kuombewa sasa, tutafurahi kufanya hivyo, kama tu ungeinua mkono wako. Kama sivyo, tutakuwa na ibada ya uponyaji mara tu baada ya. . . ujumbe mfupi; tutajaribu tu kumalizia pamoja na darasa la shule ya Jumapili. Vema. Ndipo tutasoma Maandiko na kupata Ujumbe na, upesi, halafu tuchukue muda wetu katika mstari wa maombi.

³³ Na sasa, kabla hatujaanza, ninawatakeni, wote walio wazima asubuhi ya leo, mwe mkiwakumbuka walio wagonjwa, kwa sababu hatuna budi kuombeana sisi kwa sisi.

34 Basi nilifurahi sana nilipofika California hivi majuzi, na kwenda katika zile maskani walimokuwa wakijaribu kujisukumiza. Na huko Clifton walikuwa wamesimama kwa umbali wa zaidi ya jengo la mji, huko nje barabarani, wakitaka tu kushuhudia. Na kusema, “Ndugu Branham, wakati mmoja nilikuwa na kansa. Ukaniombea. Ni—nilikuwa kipofu. Nilikuwa *hivi*.”

35 Na kama kushuka barabarani, na hisia nzuri sana! Niliwazia, “Mungu, itakuwaje tutakapovuka na kufika ng’ambo ya pili? Hao hapo, wamekusanyika kwa makumi ya maelfu, wamesimama pale.” Na litakuwa jambo la ajabu jinsi gani wakati huo! Kwa hivyo, basi, juhudi zetu ndogo za kuchosha hazitakuwa na maana sana. Sasa tunaendelea tu mpaka, inaonekana kana kwamba, hatuwezi kwenda mbali zaidi, na nusura tu kuchoka kabisa na kuanguka.

36 Ndipo Shetani anakuja, anasema, “Inafaa nini? Unaifanya ya nini?” Jamani!

37 Lakini basi ukiwazia mambo kama hayo, inayabadilisha, kabisa. Hiyo inafanya... Inafanya mambo kuwa tofauti.

38 Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu tuombe tena kwa muda kidogo.

39 Baba yetu wa Mbinguni, ni kwa mioyo yenye shukrani tunakuja Kwako. Kwa kweli, Bwana, Wewe wajua kila umbile la mwanadamu. Na jinsi alivyo dhaifu na mnyonge, na jinsi asivyo na nguvu. Na udhuru kama huo kama m—mtumishi Wako, ndivyo alivyo mwanadamu, lakini, Bwana, Wewe kwa neema Yako umetuita tuwe watumishi Wako. Nasi tunajua, asubuhi ya leo, kutostahili kwetu, nasi tunaomba ya kwamba utatukubali, Baba, leo, na utatutia mafuta kwa Roho Mtakatifu, na useme nasi Maneno ya kufariji ambayo Wewe umeyazungumza katika Neno Lako Takatifu hapa. Nasi tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataliingiza kila Neno moja kwa moja moyoni, pale tu linapohitajika kuwa, na humo naomba litie nanga na kukua likawa furaha kuu, miti ya wokovu. Tujalie, Baba.

40 Waponye wagonjwa na wahitaji. Tunajua wameketi hapa. Na wengi wametoka maili nyingi, na kulala kwenye hoteli na kadhalika, wakingojea nafasi ya kuombewa. Tuna furaha sana kwa ajili ya majaliwa haya makuu, Bwana, kujua ya kwamba Wewe uko hapa kuwaponya wagonjwa.

41 Mungu, mmojawapo wa wagonjwa sana tunaowajua, ni mwanamume na mwanamke mgonjwa wa dhambi. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba siku hii, ya kwamba Wewe, kwa namna ya pekee, utawatia mafuta, leo, na kuwaokoa waliopotea. Kila mwanamume na mwanamke aliyepotea, jalia waje kwenye Kiti cha neema kwa furaha na waokolewe, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

42 Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake, tunapoingia katika Hilo. Sikuzote nimekuwa mwaminio hodari katika Neno. Kwa maana, hapa, na siku chache zilizopita usiku, nilikuwa nikizungumza mahali fulani juu ya ma—manabii waliokwea kwenda kutabiri. Lakini, Mikaya... baada ya manabii mia nne kutoa ukuta mmoja imara. Hata hivyo, Yehoshafati akasema, “Je, hakuna mmoja tu zaidi?” Ati mmoja zaidi, baada ya mia nne kutoa Neno? Lakini, Mikaya alidumu pamoja na Neno la Mungu. Alijua kulikuwa na kasoro fulani.

43 Na mradi tunasikia chochote nje ya Neno la Mungu, tunajua kuna kasoro. Halisikiki sawa kabisa. Yesu alisema, “Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, na mgeni hawatamfuata.”

44 Na asanteni, kwa kuomba huko nje, kwa ajili ya uamsho wa Hekalu la Angelus. Jioni ya kwanza huko... Linaenea elfu tano mia tano tu; elfu tano, mia tano. Waliruhusu elfu sita kuingia, ndipo zimamoto wakafunga milango, yapata saa moja na nusu kabla sijafika huko, kwenye Hekalu la Angelus. Na jinsi mpendwa wetu Bwana Yesu alivyowaokoa waliopotea na kuwaponya wagonjwa! Ilikuwa ni ajabu. Ndipo kesho yake...

45 Naye maskini Dada yetu Hicks, ambaye alikuwa mwalimu wa shule ya Jumapili hapa, nilikutana naye na watoto wake na mumewe. Pia nikakutana na Ndugu Ben Bryant na wale wote waliotoka kwenye maskani hii, huko nje, magharibi, ku—kufanya ushirika huko nje. Ulikuwa ni kuunganika tena kwa ajabu jinsi gani, kuweza kuwaona wote tena!

46 Katika mlango wa 17 wa Mathayo Mtakatifu, kwa njia ya kusoma tu, asubuhi ya leo. Ninataka kusoma sehemu tu hapa kwa ajili ya somo. Bwana na atupe muktadha katika Neno.

... baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani,

Akageuka sura yake mbele yao, uso wake ukang'aa kama jua, na mavazi yake meupe kama nuru.

Na, tazama, akatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye.

Ndipo Petro akajibu, akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa: ninii... na tujenge... ukitaka, na tukujengee wewe vibanda vitatu; kimoja chako wewe, ... kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya.

Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli: na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependeza naye; msikieni yeye.

47 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

48 Wakati mwingine Mungu hukutana katika mashauri tofauti ya mwanadamu. Mungu sikuzote amependa kufanya shauri na mwanadamu. Na mara nyingi, katika Agano la Kale, jinsi tungeweza kurudi nyuma kutafuta jinsi Mungu alivyokutana na mwanadamu. Na bila kujali idadi yao, Mungu hukutana na mwanadamu. Alikutana wakati mmoja na mia tano. Naye alikutana, tena, na sabini. Alikutana, tena, na wale kumi na wawili. Alikutana wakati mmoja na watatu. Ndipo akakutana, tena, na mmoja tu. Na bila kujali idadi ya watu, Mungu daima hupenda kukutana na mwanadamu.

49 Kwa hivyo, ingawa kanisa asubuhi ya leo linaweza lisiwe kubwa hivyo kwa kusanyiko au katika ukubwa, kama makanisa makuu mengi leo, lakini Mungu atafurahi kukutana nasi. Kwa maana, Yeye alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Wawili ama watatu watakusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati ya hao wawili ama watatu.”

50 Na ile picha ambayo tungeweza kuweka hapa leo, kwa Roho Mtakatifu, tungeweza kuchukua saa kadhaa kuchimba ndani ya maandishi hayo, naam, ningesema kwa majuma. Na limechimbwa, kwa miaka, na, hata hivyo, nusu bado haijafichuliwa kutoka kwa maandishi haya ya ajabu, na labda kamwe hayatafichuliwa.

51 Kwa sababu, Neno la Mungu si kama neno la mwanadamu. Neno la mtu lina maana fulani, au usemi na wakati lilipotolewa, lakini Neno la Mungu lina maana ya Milele kote katika nyakati linapoendelea. Kila kizazi kinaweza kuchukua Neno lile lile, kwa sababu ni tangazo la Milele, la kudumu, lisilofikia, lililovuviwa kutoka kwa Mungu. Haijalishi kama Hilo. . . Kama mitume walilisoma katika wakati wao, lilimaanisha kitu kwao; kama Wesley alilisoma katika wakati wake, na Luther katika wakati wake, na Calvin katika wakati wake. Hata hivyo, leo, lingali ni angavu tu na linang’aa vile vile, nalo lina matokeo mengi tu kadiri lilivyofanya kwao siku ile ile liliponenwa, kwa sababu ni Neno la Mungu.

52 Maneno yetu, kusema tu, “Yohana, njoo nyumbani kwangu, nitafurahi kukuona.” Hilo ni neno letu, na linamaanisha tu, “Yohana, njoo nyumbani kwetu.”

53 Lakini Mungu anaponena, ni la Milele. Lilipumuliwa kutoka kwa pumzi yenyewe ya Muumba Mwenyewe wa milele, asiyeapatikana na mauti. Kwa hivyo, basi, hakuna njia ya kupata maana kamili ya tamshi lolote la Mungu. Ni kwa ajili ya kila wakati, na kila kizazi.

54 Sasa, katika kisa hiki, katika. . . tulicho nacho mbele yetu asubuhi ya leo, kilikuwa ni Mungu akizungumza na watu watatu mbalimbali.

⁵⁵ Sasa, *tatu*, kwanza, ni nambari iliyochaguliwa na Mungu ya “ukamilifu.” Mungu alichagua *tatu*, na *tatu* ni namba ya Mungu ya ukamilifu. *Saba* ni namba Yake ya “ibada.” *Hamsini* ni namba Yake ya “yubile.” *Arobaini* ni namba Yake ya “majaribu.” Na *tatu* ni namba Yake aliyoichagua kupanda juu, siku hii.

⁵⁶ Sasa, *tatu* ni nambari ya ukamilifu, yaani, kwamba Mungu amekamilika; Mungu yule mmoja, wa kweli, wa Milele anakamilika katika vipindi vitatu vya kudhihirishwa kwa Uungu Wake: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Haimaanishi kwamba kuna miungu watatu mbalimbali. Lakini, kuna Mungu mmoja aliyewakilishwa katika hayo matatu. Mungu sio watatu. Mungu ni mmoja. Lakini, madhihirisho matatu ya Uungu Wake, ikimaanisha, vipindi vitatu vya wakati duniani humkamilisha Mungu mmoja, wa kweli na aliye hai.

⁵⁷ Alimtokea Ibrahimu katika kichaka kilichowaka moto, na kuwaongoza wana wa Israeli, katika Jina la Mungu, Baba, ambayo ilikuwa ni Nuru iliyoning’inia juu ya maskani, iliyowaongoza katika safari yao. Mungu, Baba. Na kisha Baba, ili kuleta upatanisho kati ya Mungu na mwanadamu . . .

⁵⁸ Kama nilivyokuwa nikizungumza hapa wakati fulani uliopita, ninaamini, mara ya mwisho nilipokuwa maskanini, juu ya hua na mwana-kondoo. Jinsi ambavyo Mungu, peke yake, . . . Hakuna mtu mwingine angeweza kulifanya. Ilimbidi Mungu aje duniani na kuifanya kazi hiyo Mwenyewe. Basi alipomwakilisha Mwanawe katika umbo la mwana-kondoo, mpole kuliko viumbe vyote, na Yeye akajiwakilisha Mwenyewe katika umbo la hua, ndege mpole kuliko ndege wote warukao mbinguni. Na sababu ya kufanya hivi, ni kutuonyesha ya kwamba upole tu ndio utakaa na upole, unyenyekevu utakaa pamoja na unyenyekevu. Hauna budi kupatana.

⁵⁹ Seremala, au mtengeneza kabati, ambaye anajua maana ya kuumana, tunavyokuita, kutia mifuo, au ulimi-na-mfuo. Kuufanya ubao ukamilike, ni kuweka ulimi-na-mfuo. Na zinapoumana, zinaumana kwelikweli. Zikiwa na maji ndani yao, zingevimba hata hewa isingeweza kupenya.

⁶⁰ Basi wakati mwaminio na Mungu . . . Mungu amekamilika sana, hata, kwa kukatwa na kuumbwa kwa mwaminio, wanapokutana pamoja. Petro alisema, “Tubuni, basi, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Mnaona? Inawafanya kuwa wakamilifu sana!

⁶¹ Ndipo Mungu aliposhuka katika mfano wa hua, na kutua juu ya Mwana-Kondoo, na kukaa ndani ya Mwana-Kondoo, na kamwe hakumwacha Mwana-Kondoo, kwa maana walikuwa ni mmoja. Hayo yalikuwa ni mojawapo ya majilio makuu sana ambayo ulimwengu umewahi kuwa nayo. Hebu tuangalie tu hilo kwa muda mfupi, nje ya somo langu, lakini jinsi ambavyo

mbingu na nchi zilivyokumbatiana. Jinsi ambavyo Mungu na mwanadamu walivyopatanishwa pamoja! Jinsi ambavyo hata viumbe vinavyoruka angani, na wanyama wanaozurura makondeni, walivyofanyika kitu kimoja, wakati mwanadamu na Mungu walipopatanishwa pamoja, na Mwanadamu, Bwana Yesu Kristo. Ni jambo la ajabu jinsi gani!

⁶² Ili kukaa na Mungu, dumu mpole. Mungu ni mpole. Ili kukaa na Mungu, dumu na upendo. Mungu ni upendo. Dumu mpole. Dumu. . . Usijitegemee kamwe. Daima mtegemee Yeye. Kamwe usitumie akili yako mwenyewe; kuchukua mawazo Yake. Hebu mawazo Yake yawe mawazo yako. Na uyatie katika nia yako ya kimwili, na uyarudie tena. Na kusema, “Ee Mungu, ondoa shaka langu lote, na ujalie mawazo yangu yawe mawazo Yako.” Nanyi wagonjwa, fanyeni hivyo tunapozungumza. Ondoeni tu, ondolea mbali wazo la maradhi. Chukua mawazo ya Mungu ya uponyaji, acha Yawe wazo lako.

⁶³ “Yatafakarini mambo haya,” Biblia ilisema, “ikiwapo sifa nzuri yoyote, ukiwapo wema wowote.”

⁶⁴ Hao watatu, Mungu akizungumza nao. Sasa, tatu ni uthibitisho. Yeye aliwachukua, Petro, imani; Yakobo, tumaini; Yohana, upendo. “Imani, tumaini, na upendo, haya matatu.” Ikiwa unaweza kuwa na imani na tumaini na upendo, uko karibu na Ufalme wa Mbinguni, basi; yale mambo matatu makuu. Mungu aliwachukua hao kama uthibitisho, kwa sababu, “Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitike.”

⁶⁵ Kisha, tena, iliwakilisha kule kumweka mwana mahali pake. Katika Agano la Kale, mtoto wa kiume alipozaliwa katika familia, alipewa mwalimu wa kumlea na kumtunza. Baba alikuwa mtu mwenye shughuli nyingi sana, juu ya ufalme wake. Na kila ufalme mdogo uliitwa nyumba.

⁶⁶ Hivyo ndivyo, katika tafsiri ya King James, Yohana 14, ilisema, “Nyumbani mwa Baba Yangu mna majumba makubwa mengi.” Sasa, inasikika si sawa kwetu sisi watu wa magharibi ambao huchukua jumba kubwa na nyumba kuwa tofauti. Lakini katika siku za kuandikwa kwa Biblia, jumba kubwa lilikuwa ndani ya nyumba, kwa maana nyumba ilimaanisha ufalme.

⁶⁷ Na baba huyu alikuwa na wapangaji wengi kwenye shamba lake, kila mahali, dazani kadhaa. Basi mtoto mwanamume alipozaliwa, alikuwa na mtu aliyechaguliwa, mwenye elimu, mnyenyekevu, mtu aliyechaguliwa ambaye alikuwa mmoja aliowapenda sana, sehemu ya ufalme wake, mwalimu. Ni aina hiyo tu ambao huyo baba angeweka juu ya mwanawe.

⁶⁸ Na jinsi Baba leo hii ameweka Mwalimu anayefaa juu ya Wanawe, mimi na wewe. Mteule, si mwingine ila moyo na nafsi yenyewe ya Bwana Yesu, kutulea katika maonyo ya Mungu.

⁶⁹ Jinsi ambavyo mwalimu huyu hana budi kuchaguliwa! Hana budi kuwa mtu mwenye akili sana, mtu aliyechaguliwa, mpenzi wa baba, ambaye atamfundisha huyo mtoto kanuni sahihi pekee.

⁷⁰ Na jinsi Roho Mtakatifu, leo, akiisha kuja, mambo mengine yote yanaonekana duni Roho Mtakatifu akiisha kuja. Watu wanaweza kusema, “Siku za miujiza zimepita,” bali hebu mtu aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, wakati mmoja, aje mbele ya huyo. Kwa maana, Yeye hufundisha tu kile kilicho halisi. Ananena tu juu ya Baba.

⁷¹ Afadhali niwe na mtu ambaye hakujua ABC zake, amfundishe mtoto wangu, ambaye alikuwa na Roho Mtakatifu, kuliko maprofa wote ulimwengu wasio na Roho Mtakatifu. Kwa maana, Yeye hunena juu ya Baba. Mnaona? Naye Roho Mtakatifu hunena juu ya Baba. Na ndipo Yeye atamfundisha mtoto, “Asitupwe huku na huku na kila upepo wa mafundisho,” bali kukubali na kuamini kanuni ambazo Baba ameziweka.

⁷² Hiyo ndiyo sababu uponyaji wa Kiungu unakuwa rahisi sana, kwa mwaminio halisi, kwa sababu amefundishwa, na Roho Mtakatifu, kuamini mambo yote. Tunawezaje kutilia shaka Neno la Muumba?

⁷³ Ulimwengu ulipataje kuwepo? Je, Mungu alipata wapi nyenzo za kuutengeneza? Je, umewahi kusimama kuwazia hilo? Yeye alilineni tu. Na, hata hivyo, uumbaji wenyewe ulio hapa sasa si kingine ila Neno la Mungu lililodhihirishwa. Liwazie hilo. Miti inayokua, ni Neno la Mungu. Milima ifikayo angani, na kutufanya, endapo tunataka kuona uzuri, tutazame mlimani. Na kadiri unavyopanda juu mlimani, ndivyo huo unavyozidi kuwa mkamilifu na safi zaidi.

⁷⁴ Unaposimama kule kwenye uwanja wa barafu wa kaskazini mwa British Columbia! Unapotazama hapa, kwenye kinamasi; juu kidogo, maji ni safi, yanakuwa bluu zaidi na safi zaidi, miti inatoweka. Maumbile yote yanaonekana kusema, “Angalieni juu.” Na juu kabisa ya theluji kuu iliyojaa barafu ambayo inang’aa sana hata inang’aa kama jua, unatazama juu. Ikiwa unataka kuona vitu vizima na vya kweli, na vitu safi, daima angalia juu. Mlima unaelekeza kwake. Daudi alisema, “Nitatazama milimani ambako msaada wangu unatoka. Msaada wangu unatoka kwa Bwana.”

⁷⁵ Huyo mwalimu sikuzote alimwelekeza mtoto kwa baba, na kulazimika kumwamini baba. Na, basi, huyo mwalimu alikuwa mkufunzi.

⁷⁶ Asubuhi ya leo, nilipokuwa nikimtaazama maskini mwenzangu mpendwa, kisha nikamwona mwanangu mdogo, wakati aliposhikwa na maskini hamaki yake mezani, pamoja na bakuli yake na mayai yake na kadhalika, mama huyo alikuwa amefanya kazi kwa uaminifu sana kuyapika kwa ajili

ya kiamshakinywa chake. Naye alikuwa akijaribu kumfundisha kula kwa kijiko chake. Basi alitaka kutumia mkono usiofaa.

⁷⁷ Vema, kwangu mimi, nilisema, “Mwache atumie mkono huo.” Lakini mama alijua vingenevyo. Alijua, kama angemwacha aendeleo hivyo, angekuwa ama stadi wa kutumia mikono miwili au angekuwa wa kutumia mkono wa kushoto, na hiyo si kawaida. Kwa hivyo, kama mkufunzi wa kweli, alimfanya abadilishe mkono, ingawa hakupenda. Lakini, mama alijua lililo bora zaidi.

⁷⁸ Na mara nyingi, mkufunzi wetu, Roho Mtakatifu; tunajaribu kulifanya kwa njia isiyofaa. Lakini, wakati mwingine linatumiza. Wakati mwingine tunaweza kulala kwenye kitanda cha mateso. Wakati mwingine daktari anaweza kusema kwamba matumaini yote yamekwisha. Lakini, ni Roho Mtakatifu akitufundisha kutumia mkono wa kulia. Anajua kilicho bora zaidi. Anajua jinsi Baba anavyotaka ifanywe. Yeye ndiye mkufunzi. Basi nilifikiri. . .

⁷⁹ Mtoto Joseph, hakutaka kuutumia huo mkono, kwa hiyo mama ananyoosha mkono na kuchukua maskini fimbo yake ndogo nyepesi, yapata urefu huu, naye akaipigapiga pembeni. Akanitazama. Lakini, hata hivyo, nilimpenda kwa moyo wangu wote, ningekufa bure kwa ajili yake, lakini nilijua mama alijua vyema zaidi. Nikasema, “Anamfundisha mtoto.”

⁸⁰ Hatuwezi kutazamia huruma, na kuhurumiwa, kupita kiasi. Inatubidi kusikiliza mafunzo ya watoto ya Baba yetu. Anajua kilicho bora zaidi. Wakati mwingine tunasema, Injili inapohubiriwa, “Loo, nitaenda tu kanisani kwangu, hawaninii. . . Naam, nitaliamini tu *hivi*.” Mnaona? Lakini, kumbuka, Roho Mtakatifu anajua vyema zaidi. Anajua jinsi ya kukufundisha. Wakati mwingine anagongagonga kwa fimbo, anakurekebisha. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Lazima ukumbuke, Mungu alimfanya Yeye m—mkufunzi wa watoto kwa ajili ya Kanisa. Naye anampenda Baba, Naye daima ataelekeza kwa Baba.

⁸¹ Na, sasa, mtoto alipokuwa akijizoeza, hiyo haikumaanisha huyo mtoto. . . Huyo mtoto hakika ni mtoto wa baba. Lakini iwapo alikuwa ni mtoto asiye mtiifu, mkufunzi sikuzote atakuwa na shida naye. Daima, alikuwa akiingia na kutoka, huku na huku. Vema, basi, ilibidi ujumbe huu uletwe kwa baba, wakati baba alipohitaji. “Mtoto wangu anaendeleaje?”

⁸² Basi itambidi kusema, “Haendelei vizuri sana.” Vema, basi, bila shaka, hilo liliuhuzunisha moyo wa baba.

⁸³ Na linafanya hivyo siku hizi, wakati Roho Mtakatifu hana budi kuleta kumbukumbu zetu mbele za Mungu. Tunapofanyika watoto wa Mungu, tunapaswa kuenenda inavyostahili huo wito. Tunapaswa kutembea inavyostahili kila kitu ambacho Mungu

ameweka kwa ajili yetu kufanya. Kwa maana Roho Mtakatifu anatumfundisha, mafunzo ya mtoto. Je, uliwahi . . .

⁸⁴ Nilipokuwa mvulana, baba yangu alikuwa tofauti na baadhi ya baba wa kisasa walivyo siku hizi. Baba yangu aliamini katika kucharaza viboko, na kwa kweli alicharaza. Tulivikumbuka. Nami, hata hivyo, leo hii, nikiwa na miaka arobaini na saba, ninavikumbuka. Lakini vilinisaidia. Vilinifundisha. Kama ningeweza kwenda kaburini leo na kumfufua, jambo la kwanza ningefanya ni kumsalimia kwa mikono na kumkumbatia kwa kile alichofanya.

⁸⁵ Kama nikijisikia hivyo kuhusu baba yangu wa duniani, itakuwaje siku hiyo tutakaposimama katika Uwepo Wake? Wakati, tutakapooa mambo yakitukia kwa manufaa yetu, kwamba ilimbidi atukate kidogo hapa, na kutupa mafunzo ya mtoto, na kuyaondoa mambo ya ulimwengu, na kutufanya tutembe kama watoto wanyenyekevu mbele Zake. Inaweza kuonekana kuwa ngumu mwanzoni, lakini Mungu anajua anachofanya. Hakika. Anajua anachofanya.

⁸⁶ Naye, basi, Roho Mtakatifu anapoanza kuleta Neno, basi, ikiwa mtoto hajawa mtiifu wakati anapopevuka, umri wa kupevuka, basi, huyo mtoto daima ni mwana, bila shaka, lakini anapoteza kitu fulani.

⁸⁷ Basi hii hapa hoja ninayotaka kuwaelevesha barabara. Roho Mtakatifu na aipeleke kwa kila moyo wa ninyi waaminio. Kwa sababu tu wewe ni mwaminio, bila shaka una Uzima wa milele; Mungu alisema hivyo. Lakini ungependa tu kuingia, kama Ayubu alivyosema, “Kwa ngozi ya meno yako”? Je, ungetaka kuja tu mbele za Baba, na kipaji ambacho amempa kila mmoja wenu, kwamba ulizembea, kamwe hukukitumia, au uliacha kitu kingine kikuzuie? Uliachilia vitu vidogo vidogo visivyo na maana yoyote kwako, hata hivyo, ugomvi mdogo, na kuzozana, na mabishano, na tofauti za kanisa, ziondoe upole na unyenyekevu maishani mwako. Je, ungetaka kusimama mbele za Baba namna hiyo? Siamini ungetaka. Siamini kwamba ungefanya hivyo. Wala mimi.

⁸⁸ Jinsi ninavyotaka aseme, “Ulifanya vema sana.” Sio kwa ngozi ya meno yangu; lakini, “Ulifanya vema sana, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu. Ingia katika furaha za Bwana, kwa kuwa ulifanya vema kwa yale uliyopewa kufanya.”

⁸⁹ Labda wewe ni mke wa nyumbani. Ikiwa ndivyo ulivyo, Mungu alikufanya mwalimu wa watoto wako. Fanya kazi nzuri kwake. Haidhuru unapaswa kufanya nini, lifanye vizuri.

⁹⁰ Angalieni, basi, kama mtoto huyo alithibitika kuwa kweli alistahili vitu ambavyo baba alikuwa navyo juu ya ufalme wake, naye alikuwa mtoto mwaminifu kweli, basi mwalimu alileta ujumbe kwa baba, “Loo, mwanao . . .”

⁹¹ Loo, sasa, huo ndio ujumbe ninaotaka Yeye alete kwa ajili yangu na yako. “Loo, Mwanao, mawazo yake yote yako juu Yako. Yote anayotaribu kufanya ni kukupendeza Wewe. Anavutiwa sana na mambo Yako, hata ni vigumu kumzuia.”

⁹² Afadhali niwe na bidii kupita kiasi kidogo juu ya Ufalme wa Baba kuliko kutokuwa na bidii hata kidogo, kwa ajili Yake. Afadhali nifanye kazi kupita kiasi. Na kama vile mhubiri wa Church of Christ alivyoniambia, siku moja, “Bw. Branham, afadhali—afadhali nichakae kuliko kuingia kutu.” Na huo ni ukweli mwingi. Afadhali nichakae, “na kufia kazini,” kama Ndugu Neville alivyosema, kuliko kukataa kuingia kazini. Huwezi kufanya kufanya lolote baya zaidi kuliko kupuza kujaribu. Hebu tufanye yote tuwezayo kwa yale unayopaswa kufanya nayo. Naye Roho Mtakatifu, Mwalimu wetu, atalileta kwa Baba.

⁹³ Na sasa, angalieni, kama mtoto huyo akiwa mtoto hodari, basi baba alipashwa habari. Na kwenye... Loo, nalipenda Neno kweli! Kwa wakati uliowekwa, uliowekwa na baba peke yake, huyo mtoto alikuwa... utukufu na heshima yake ilidhihirika mbele ya umma. Baba akamchukua mtoto wake mwenyewe, chini ya sherehe, na kumpeleka mahali pa hadharani. Baada ya ninii yake... Akiwa ni mtoto wake mwenyewe, alieyazaliwa katika nyumba yake mwenyewe, hata hivyo, huyo mwana aliwekwa mahali pake katika familia, kurithi vitu vyote alivyokuwa navyo baba. Mnaliona?

⁹⁴ Sasa, kama tutakuwa na tabia njema, siku moja tukufu tutarithi mambo yote. Mungu, katika siku Yake aliyoamriwa, kwamba atawahukumu watu wote kwa Kristo Yesu. Wakati utakuja ambapo Mungu atatoa thawabu kwa wale waliokuwa waaminifu, na kukataliwa kwa wale wanaokosa kuwa waaminifu.

⁹⁵ Kabla tu ya kuondoka kwa Bwana Yesu... Mungu akiwa ndani Yake; Hua akimwongoza Mwana-kondoo. “Hakuja kufanya mapenzi Yake mwenyewe, bali kufanya mapenzi ya Baba aliyemtuma.” Aliongozwa na Roho, kuwatwaa Petro, Yakobo na Yohana, hadi kwenye mlima huu mrefu sana. Napenda hilo!

⁹⁶ Na, jambo lingine, ikiwa mtanisamehe kwa kuchukua muda mwingi, bali nataka kuweka mbele ya wasikilizaji hawa asubuhi ya leo, ya kwamba hili lilikuwa na maana nyingine kwake. Baada ya kutoka mlimani na kushuka, swali liliulizwa, “Watu husema Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Ati nani? Watu wanasema nini kunihusu Mimi? Kwa vile Mimi niko pamoja nanyi, na nimedhihirishwa kwenu, sasa watu wanasemaje juu Yangu Mwana wa Adamu?”

⁹⁷ Litazameni. Ni picha nzuri jinsi gani ya siku hizi! Ukiisha kumpokea Kristo, ukiisha kujazwa na Roho, watu wanasema

nini juu yako basi? Watu wanasema nini, wanapoona mihemuko yako imechochewa sana hata huwezi kutulia, machozi ya furaha yatatiririka mashavuni mwako, wakati huwezi kuweka mikono yako chini wakati wanaimba nyimbo za Sayuni; wakati huwezi kunyamaza, unapoona dhambi na huna budi kuzungumza nao kwa amani na utulivu? Watu wanasema nini juu yake? Watu wanasema nini, wakati umelala, ukifa, mwenye mashaka, mnyonge, katika hali ya kufa, nawe unamwomba mtoto fulani wa Mungu aungane nawe katika maombi kwa ajili ya uponyaji wako; nawe unaungama makosa yako na kuweka hicho kitu mbele za Baba, useme, “Baba, nisamehe, na sasa ninamkubali Kristo kama mponyaji wangu,” nawe unaponywa?

“Watu husema Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

⁹⁸ Ninatazama kusanyiko la watu, na baadhi yenu ninawajua; wenye mashaka, miaka kadhaa iliyopita, mkifa kwa kansa, hatua ya mwisho. Baadhi yenu katika hali za kila namna, sura, vipofu. Na Mungu, kwa neema Yake, akakuponya. Basi unapotoa ushuhuda wako wa ushujaa mbele ya watu . . .

“Je, watu wanasema kwamba mimi Mwana wa Adamu . . .?”

⁹⁹ Walisema nini juu yake? Jinsi picha hata imebadilika kutoka siku hiyo, ingawa ni nyeusi kadiri ilivyokuwa! Wengine wanasema, “Ni ulokole.” Wengine walimwita, “Beelzebuli.” Wengine wanasema, “Ni telepathia ya kiakili.” Wengine wanasema, “Ni msisimko.” Wengine wanasema, “Ni ulokole.” Wengine wanasema, “Ni mhemuko.”

¹⁰⁰ “Lakini mnasemaje kulihusu? Mnasemaje kuhusu jambo hili?”

¹⁰¹ Petro mwenye kiherehere kwa kawaida huzungumza kabla ya zamu yake, lakini wakati huu hakufanya hivyo. Alisema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Sijali hao wengine wanasema nini. Hivyo ndivyo ni juavyo. Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

¹⁰² Sikilizeni. Tungeweza kutumia muda mwingi hapo. Lakini hebu tuendele. Yesu alisema, “Heri. . .” Ingawa watu wanaweza kulaani, ingawa watu wanaweza kufanya mzaha. Watu wanaweza kusema wewe ni mtakatifu anayejibingirisha. Watu wanaweza kukuita jina lolote chini ya jua. Lakini Yeye alisema, “Heri wewe, Simoni Bar-yona. Baba yako . . .”

¹⁰³ Hili hapa sasa. Mko tayari? “Kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza hili kupitia seminari fulani ya mafundisho ya sharti. Wala hukujifunza kutokana na azimio fulani la theolojia ya mtu fulani. Mwili na damu havijakufunulia hili, lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili.” Unaona unakotoka? Kupitia kwa Mwalimu, Roho Mtakatifu, amelifunua kwa ufunuo.

¹⁰⁴ “Nami nakwambia, wewe ndiwe Petro, jiwe dogo. Mimi ndimi Mwamba mkuu. Mimi ndimi Jiwe la Pembeni, lakini wewe ni jiwe dogo lililowekwa juu Yangu. Wajenzi walikuchagua. Hukujichagua mwenyewe. Wajenzi walikuchagua. Malaika wa Mungu, usiku mmoja, wakifanya kazi kwenye machimbo ya mawe, walikuita utoke, nawe ukajisalimisha Kwangu. Nami nikakukata kwa mtindo Wangu. Nilikufanya jinsi nilivyotaka uwe. Nilikukata kwa msumeno; ukasimama tu kimya. Nami nimekuweka sasa kama jiwe dogo, upate kuumana na jiwe jingine, kuliongoza jiwe hilo; na jiwe *hili* huongoza jiwe *hilo*, jiwe *lile*. Nayo saruji ya upendo inawaleta ninyi pamoja, kufanya Msingi, ambao ni Mimi, kuunganishwa pamoja na kila jiwe linalokiri Jina Langu na kupokea ufunuo huu.”

¹⁰⁵ “Na juu ya mwamba huu, ufunuo wa Mungu, ambao utasimama kimya na kukatwa, (hilo jiwe, kwa ufunuo), nitalijenga Kanisa Langu, na malango yote ya kuzimu hayatalishinda.” Ikionyesha kwamba, kwa hakika, malango yote ya kuzimu yatakuwa dhidi yake, lakini hayatashinda kamwe.

¹⁰⁶ Na hebu nichukue wakati huu kusema haya, rafiki yangu, kwamba, Kanisa lote la Mungu aliye hai limejengwa kwa uchaji juu ya ufunuo wa kiroho wa Bwana Yesu Kristo. Haidhuru umesoma kiasi gani, jinsi ulivyo mweru, jinsi unavyoweza kufikiria unaijua Biblia vizuri, Shetani anaijua vizuri zaidi kuliko wewe. Lakini ni kwa ufunuo tu, Mungu kupitia Roho Mtakatifu, Mwalimu wako, alikufunulia, kwamba Yeye anakuokoa kwa neema Yake.

¹⁰⁷ Kama atakufunulia asubuhi ya leo, kwa ufunuo, ya kwamba huu ndio mwisho wa mateso yako, huu ndio mwisho wa maradhi yako, ibilisi wote kutoka matesoni kamwe hawatautikisa msingi huo, ingawa kila daktari anasema si sahihi. “Kwa maana juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, nayo malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

¹⁰⁸ Ingawa yatakuwa dhidi yake, hata hivyo hayawezi kushinda. “Kwa maana adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu atainua kiwango dhidi yake,” kila wakati. Mnaliona? Mnalipata? Sasa, Yesu, akifunuliwa kwa wanafunzi.

¹⁰⁹ Angalieni katika bustani ya Edeni, wakati Kaini alipoleta dhabihu katika ibada, kama vile Habili alivyofanya. Aliabudu. Alililipa kanisa. Alijitolea. Alifanya kila tendo la kidini, angavu zaidi, lililofaa zaidi, kuliko alilofanya Habili. Alijenga madhabahu bora zaidi. Aliifanya kuwa nzuri zaidi. Aliweka madoido kwenye ibada yake. Unaona ukoo huo ungali ukifanya kazi miongoni mwa wana wa Adamu? Aliweka madoido kwake, pamoja na matunda ya kondeni, na yungiyungi kubwa. Na, si hayo tu, bali aliabudu. “Iko njia ione kanayo kuwa sawa kwa mwanadamu.” Lakini, alichofanya, aliabudu kwa njia ya maarifa. Hakuabudu kwa ufunuo.

¹¹⁰ Basi inawezekana. Lishikeni sasa. Sikilizeni. Unaweza kuabudu kwa njia ya maarifa. Unaweza kwenda kanisani, kwa kujua kwamba unapaswa kufanya hivyo. Lakini kwenda kanisani, kwa njia hiyo, ni kuabudu bure. Lakini wakati kuna kitu kimefanyika moyoni mwako, kinachokufanya umpende Mungu, hivi kwamba huwezi kukosa kwenda kanisani, huo ni ufunuo, Mungu akifunua.

¹¹¹ Hawakuwa na Biblia wakati huo. Hawakuwa hata na karatasi wala sleti ya kufanyia kazi. Hawakuwa na shule za elimu. Kwa hiyo, Habili, kwa ufunuo, alifunuliwa na Mungu, kwamba, “Haikuwa urembo, wala haikuwa matunda ya kondeni, wala matofaa, ambayo yaliwafukuza kutoka katika bustani ya Edeni, lakini ilikuwa ni damu.” Basi ilifunuliwa kwake, naye akaenda akachukua mwana-kondoo. Kwa ufunuo, alitangulia kuona Kuja kwa Mwana-Kondoo Mwenye Haki. Na ilifunuliwa kwake, kwa hiyo akamchukua mwana-kondoo. Na kwa ufunuo, akamtolea Mungu, ndipo akakubalika. Kanisa zima limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho. Ni zuri jinsi gani!

¹¹² Sasa, tunakaribia kufunga. Walikuwa mlimani. Na baada ya Yesu kuwa Mtoto mtiifu; ule mwili, Mwana-Kondoo, alikuwa ameongozwa na Roho Mtakatifu, Mungu akitenda kazi ndani Yake. “Sikuja kufanya mapenzi Yangu, bali mapenzi Yake aliyenituma. Na Yule aliyenituma, Baba aliyenituma, yuko pamoja Nami. Na kama vile Baba alivyoenituma, naye akaenda pamoja Nami, Mimi nami nawatuma ninyi.” Sio tu kwamba alituma, bali alikwenda pamoja Naye.

¹¹³ Naye Mungu hamsomeshi mtu tu na kumtuma na azimio la ujuzi fulani wa seminari. Lakini, kama amefanyiwa maandalizi, Mungu huenda pamoja naye. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

¹¹⁴ Angalieni, linapendeza, loo, jinsi Neno linavyoenda pamoja! Jinsi Roho Mtakatifu anavyoliimarisha mioyoni mwa watu, kwa ufunuo na upendo wa Bwana Yesu. Angalieni kwa makini.

¹¹⁵ Huko, baada ya utii, “kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu,” mashahidi bora sana waliopata kusimama juu ya ardhi. Upendo... Petro, Yakobo na Yohana; tumaini, imani, upendo. Chini ya mashahidi wa tumaini, chini ya mashahidi wa imani, chini ya ushuhuda wa upendo; Mungu alimweka Mwanawe, mahali pake, hadharani, mbele ya hayo madhihirisho yote matatu makuu zaidi (tumaini, imani na upendo) ambayo ulimwengu utawahi kujua.

¹¹⁶ Na, pale, kama vile baba zamani za kale alivyomtoa mwanawe nje na kumvika joho, na kufanya sherehe, ndipo baada ya hapo jina la mwana lilikuwa sawasawa na la baba. Huyu mwana alikuwa mrithi wa vitu vyote.

¹¹⁷ Naye Mungu alimpeleka Kristo juu ya mlima wa kugeuka sura, kwa ushahidi wa tumaini, imani na upendo, na kumtia

uvuli kwa Wingu. Nayo Biblia ilisema, “Mavazi yake yaling’aa kama jua. Na Sauti kutoka Mbinguni, ikasema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa.’”

¹¹⁸ Sasa, Petro alisisimkwa sana, kama kawaida. Alikuwa mtu mwenye bidii sana. Na laiti sisi sote tungekuwa na bidii; mara nyingi unaweza kusema mambo mema katika harakati zako za bidii. Lakini Petro alishikwa na shauku sana alipoona kilichotokea hasa. Mungu alikuwa atamwacha awe na ushuhuda katika muda mfupi tu, baada ya wao kushuka. Lakini alipoona, amesimama... Kulikuwako na watatu hapa: tumaini, imani, na upendo. Na kulikuwa na watatu wamesimama kule mlimani: Petro, Yakobo, na Yohana, *hapa*. Musa, Eliya, na Kristo, wakisimama *pale*, katika uthibitisho wa hawa watatu hapa. Sasa, walitazama. Huyu hapo Musa amesimama, kwanza; wa pili alisimama Eliya, nabii.

¹¹⁹ Nao watu wengine wanatuuliza, “Tukifika huko tutafahamiana?” Wakati, Eliya na Musa walikuwa wameondoka, mamia mengi ya miaka. Sio tu kwamba tutafahamiana, tutawajua ambao hatujawahi kuwaona. Petro, Yakobo na Yohana walikuwa hawajamwona Musa, hata hivyo waliwatambua kufumba na kufumbua jicho, walipokuwa wamesimama chini ya Kivuli cha Mwenyezi. Itakuwaje tutakaposimama Kule? Nitamjua Sankey nikimwona. Nitaijua sauti yake, ingawa sikuwahi kumsikia. Nitamjua Wesley. Nitawajua Moody, Calvin, Knox. Tutawajua wote tutakapofika huko. Tutachukua hali tofauti na ile tuliyo sasa. Tutakuwa katika ninii isiyodumu... au—au, katika hali ya utukufu. Petro, Yakobo, na Yohana walikuwa hivyo. Kwa hiyo, katika utangulizi huo, kama wangeweza kuwatambua watu, pasipo na kosa moja, ambao hawakuwahi kuwaona au kuona picha yao, ambao walikuwa wameondoka kwa mamia ya miaka; lakini, katika utangulizi, angeweza, katika dakika moja kuwatambua, bila shaka; itakuwaje tutakapotukuzwa, tukisimama katika Uwepo Wake? Je, tutafahamiana? Bila shaka. Tutamjua kila mtu. Sehemu ndogo ya kutokuwa na kikomo itakuja juu yetu, kama vile Mungu asivyo na kikomo.

Angalieni. Sina budi kufunga. Walipotazama, kisha Petro...

¹²⁰ Kama vile mwanafunzi mzuri wa seminari angesema, “Unajua, ninaamini makanisa yote ni sahihi. Ikiwa wewe ni sahihi katika imani yako, haijalishi, kwa hivyo tutakuwa na Waislamu na Wabudha, na tutawaleta wote pamoja.”

¹²¹ Petro alisema, “Ni vizuri sisi kuwa hapa, basi hebu sasa tujenge vibanda vitatu. Tutajenga seminari hapa ya Musa. Tutajenga seminari ya Eliya. Na wote wanaotaka kuabudu chini ya torati, na kadhalika, acheni waabudu.” Na sasa tunaona.

Wakatazama, ndipo Petro na wao, wakimtazama Musa. Musa aliwakilisha torati.

¹²² Mungu aliwapa wana wa Israeli torati kwa sababu walitaka torati. Mungu hakutaka wawe nayo. Hilo ni chaguo la mwanadamu. Katika Kutoka 19, wao walisema, “Tupe kitu cha kufanya, ili tuustahili wokovu wetu. Tutashika sheria, kama utatupatia,” kwa maneno mengine. Lakini, kamwe haukuwa ni mpango wa Mungu.

¹²³ Ni bora tu kuacha kupanga, wewe mwenyewe, na kutumia tu mpango Wake. Ninaona hilo kuwa rahisi zaidi, kuchukua mpango Wake.

¹²⁴ Huyu hapo Musa amesimama, torati. Petro akasema, “Vema, baadhi yetu tunashika sheria.” Sasa, hakuna mwenye mwili anayehesabiwa haki kwa sheria.

¹²⁵ Kwa hiyo, baadaye, baada ya torati ya Mungu kusimama pale; anayefuata, aliyesimama, alikuwa ni Eliya. Ndivyo walivyokuja, kwa mfuatano wa nambari. Aliyefuata, aliyesimama, alikuwa ni Eliya, aliyemfuata Musa. Naye Eliya aliwakilisha haki ya Mungu, manabii. Naye Eliya aliwakilisha haki Yake, kwa kuwa Eliya alishusha moto kutoka mbinguni na kuwaua wale hamsini. Naye alikuwa akiwakilisha haki ya Mungu.

Kwa hiyo, Petro alitaka sheria ya Mungu na haki ya Mungu.

¹²⁶ Hakuna mtu anayeweza kuokolewa kwa sheria. Na kama ukishindwa, kuvunja sheria, kuna kitu kimoja tu kilichosalia, nacho ni kifo. Hiyo ndiyo haki ya Mungu. Mungu—Mungu anahitaji hilo. Sheria Yake ya haki lazima iwe . . . iwe na haki.

¹²⁷ Kwa hiyo, basi, Petro alipokuwa akizungumza, akitaka kujenga maskani yake, na kumwuliza Mungu kama angeweza kufanya hivyo, ndipo walipotazama nyuma wakamwona Yesu peke yake.

¹²⁸ Torati ilikuwa imeshindwa. Hebu sisi, asubuhi ya leo, tuondoe macho yetu kutoka kwenye kujihesabia haki, ama jambo fulani ambalo tumefanya. Siombi sheria. Siwezi kuhukumiwa kwa sheria, kwa sababu mimi sina sheria. Hakuna mtu aliyeshika sheria. Hawakuweza kushika sheria.

¹²⁹ Na wala huwezi kujiokoa mwenyewe. Wala huwezi kujiponya mwenyewe. Na kama sheria, kwa mapenzi yako mwenyewe ya kujibunia, ulitaka kuonyesha hayo kwenye ule mpangilio, basi kuna jambo moja tu linalohitajika na sheria, ukishindwa, hilo ni haki. Na, haki, ni kuhukumiwa na kufa milele. Inahitaji maangamizi makamilifu. Kwa sababu, anayevunja nukta moja ya torati ana hatia ya torati yote. Kwa hiyo, huna budi kufa, bali Mungu . . . tunapoitazama sheria ya Mungu, na tunatazama haki ya Mungu.

¹³⁰ Hebu tutupe macho yetu upande mwingine. Tuangalie *hapa*. Huyu hapo amesimama Yesu, akiwakilisha upendo wa Mungu. Si torati, si haki, lakini ndani Yake ulitimizwa utimilifu wa sheria na haki pia. “Huyu ni Mwanangu mpendwa.” Hakuna vitu vya kujibunia tena. Msikilize mwalimu wako. Hiyo ndiyo sababu Petro angeweza kusema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.” Torati na haki zilitimizwa katika Kristo, na ni upendo wa Mungu kwa wanadamu. Upendo wa Mungu! “Mungu aliupenda ulimwengu sana!”

¹³¹ Mungu mwenye rehema, asubuhi ya leo, ninapolitetea kusanyiko hili, hatuitetei torati, hatuombi torati yoyote. Hatutaki kuhukumiwa kwa ustahilifu wao wenyewe. Sitaki haki Yako, Bwana. La, si hukumu Yako kunijia; hashu, Bwana. Lakini, naomba rehema Zako.

¹³² Alisema, “Msikieni Yeye.” Kwa nini nimsikie? Ndiye pekee aliye na wokovu. Mariamu, Yusufu, na watakatifu wengine wote walikuwa watu wakuu, lakini Yeye pekee. “Msikieni Yeye.” Yeye ndiye mwombezi pekee. Yeye ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, ni Kristo Yesu.

¹³³ Kwa nini nimsikie Yeye? Torati isingeweza kunipa amani; Yeye anaweza. Haki isingeweza kuniletea chochote, ila hukumu. Yeye ananipa amani na upatanisho. Sheria ingeweza kunihukumu, kwa sababu, nikiwa mgonjwa, sheria inanihitaji niwe nazo zote mbili, kanuni za maumbile na haki ya Mungu, zinawekwa juu yangu, kwa hivyo sina budi kuilipia adhabu. Lakini ninageuza mapenzi yangu na macho yangu, asubuhi ya leo, kutoka kwenye sheria na haki pia, na kuangalia upendo wa Mungu aliyenipatanisha tena Kwake, kwa njia ya neema, wala si kwa njia ya sheria na kwa njia ya haki. Lakini, kwa njia ya upatanisho, Yeye alilipa gharama ya kumleta mwanadamu na Mungu pamoja, kuwafanya kuwa kitu kimoja.

¹³⁴ Huko Uswisi, si muda mrefu uliopita. . . Ninapofunga kwa tamshi hili. Wengi wenu ninyi watoto shuleni, nadhani bado mnayo, ile hadithi ya kale ambayo haipaswi kufa kamwe. Ingawa, siku hizi inafifia, nchini mwetu, lakini kamwe haitafifia huko Uswisi ambako ilitokea. Je, mnakumbuka katika shule yenu, katika kitabu chenu, Arnold von Winkelried, yule shujaa mkuu wa Uswisi? Unaweza kutaja jina lake, leo, huko juu katika Milima ya Uswisi, na nyuso zao zitapauka na machozi yatatiririka mashavuni mwao. Miaka mingi iliyopita. . .

¹³⁵ Waswisi ni watu wanaopenda amani. Ni Wajerumani ambao, huko nyuma katika karne za mwanzoni, walishuka chini milimani ambako hakuna mawe ya madini wala chochote. Lakini walinunua. . . Wana akili za Wajerumani. Wajerumani wanadhani wao ndio jamii bora, ni kweli, lakini anajaribu kuvumbua bunduki au bomu litakaloshinda dunia nzima kwa akili zake. Lakini Mswisi ni mtu anayependa amani.

Anashuka na kujifanyia ninii. . . anajitwalia nyenzo fulani, na kumtengenezea jirani yake saa, na kuishi kwa amani.

¹³⁶ Kisha, huko juu kwenye milima mirefu ya Uswisi, miaka mingi iliyopita, walipoanzisha ufalme wao—wao, au ningesema serikali yao, hawakuwa taifa la kijeshi. Walikuwa taifa linalopenda amani.

¹³⁷ Basi siku moja, wakati wavamizi walipokuja kwenye nchi yao na walikuwa wakikanyagia chini kila kitu walichokuwa nacho; hakuna, hakuna, haijalishi walijenga nini. Walibingirisha mawe chini ya milima, na kamwe haikuwasumbua. Nao walikuwa wamelisukuma jeshi la Uswisi uwanjani chini ya mlima.

¹³⁸ Nao Uswisi ni mzuri, jinsi nimewatazama, jinsi wanavyolima; na kwenye nchi tambarare; na wanaofuata ni ng'ombe, kisha juu zaidi ya mlima ni kondoo, na huko juu kabisa ndiko wanakofuga mbuzi wao.

¹³⁹ Na jinsi walivyo na zile nyimbo za kiyodeli ambazo hawa wanaojiita yodeli wa Hollywood ya Marekani wanazifanyia mzaha, kamwe hawalingani nazo. Jinsi walivyopiga baragumu zao wakati wa shida, hata, na kila jirani wakakusanyika haraka pamoja kusaidia wakati kulipotokea haja. Na sasa tunazitumia kama bendi ya jazi, roki. Loo, ni ninii sana. . . Uchafu mtupu!

¹⁴⁰ Sikilizeni, enyi marafiki. Nitatoa tamshi la meneja wangu: “Ikiwa Mungu hataleta hukumu haraka kwa kizazi hiki cha watu wazinzii, itamlazimu kuinua Sodoma na Gomora, na kuomba msamaha kwa kuiteketeza.” Hiyo ni kweli. Bila shaka. Yeye ni mwenye haki, wala hakuna kitu kingine kinachoweza kufanywa pasipo Mungu kukifanya. Na wakati rehema imefungua mikono Yake, ikimbilie.

¹⁴¹ Na kule, juu mlimani, ambapo jeshi hili dogo lilikuwa na silaha zozote walizoweza kupata, za ngao, na fimbo, na visu vya misumeno, na chochote kile walichokuwa nacho, na uma za nyasi. Wamesukumwa nyuma, lile jeshi kuu la kigeni likaja kama ukuta thabiti wa matofali. Walikuwa kila mtu amefunzwa, na mikuki mikubwa, nao wakaendelea mbele, karibu, wakilisukumia mlimani maskini jeshi hili la Uswisi. Hawakuwa na matumaini. Kila kitu walichokuwa wamejaribu kilikuwa cheusi na giza, wala hakuna kitu kilichoweza kuwaokoa.

¹⁴² Baada ya kitambo kidogo, kutoka katikati yao, kikasikika kilio cha mtu mmoja, Arnold von Winkelried. Naye akajitokeza nje, akasema, “Ndugu zangu, leo hii nafa kwa ajili ya Uswisi na kwa ajili ya uhuru wake.” Akasema, “Tunaipenda nchi yetu na yale ambayo baba zetu wamepigania, na yale ambayo baba zetu walikusudia tuwe nayo. Na, leo hii, uchumi wetu mkuu uko hatarini. Basi leo hii nayatoa maisha yangu bure kwa ajili ya Uswisi.” Akasema, “Huko, nyuma ya mlima, kuna nyumba

yangu nzuri, na mke wangu mwema mpendwa, na watoto wangu wadogo, wakinitarajia kurudi. Lakini,” kasema, “Sitawaona tena katika dunia hii.” Akasema, “Leo hii, nitakufa kwa ajili ya Uswisi.” Yeye. . .

Wakasema, “Utafanya nini, Arnold von Winkelried?”

¹⁴³ Akasema, “Nifuateni. Nitavunja safu za lile jeshi. Nitavunja ngome yao. Na kisha ninyi mnyakue chochote mlichio nacho, na kupiga vita vizuri mwezavyo. Kama mtu wa vita, piga vita kwa kile ulicho nacho, vizuri uwezavyo.”

¹⁴⁴ Basi akainua mikono yake juu, kisha akaangalia huku na huku ambako wingi wa mikuki ulikuwa ukitokea, huku akisogea kidogo kidogo. Kisha akainua mikono yake na kupiga mayowe, “Fungua njia kwa ajili ya uhuru!” Ndipo akatimua mbio kuelekea kwenye ukuta huo wa matofali uliokaribia. “Fungua njia kwa ajili ya uhuru!” akasema kwa sauti kuu. Naye akakimbilia penye msitu mnene zaidi wa mikuki, akaikumbatia ile mikuki, akaichomeka kifuani mwake, akafa. Nao wale Waswisi, walipokuwa wakimfuata, pamoja na walichokuwa nacho. Ilisababisha msisimko mkubwa sana, mpaka ukavunja safu yao. Kila mtu alikuwa nje ya mahali pake; hawakujua la kufanya. Basi Waswisi wakakimbilia mle na kupata ushindi, na Uswisi haijawahi kuwa na vita tangu wakati huo. Itakumbukwa kwa muda mrefu nchini Uswisi, almuradi kuna Uswisi, Arnold von Winkelried atakumbukwa.

¹⁴⁵ Lakini, huo ni ushujaa wa kushangaza, mnaona, haujawa na kifani, lakini ni jambo dogo, jambo dogo tu, ukilinganisha na siku moja wakati wana wa Adamu. . .

¹⁴⁶ Wakati torati ilipokuwa imeshindwa, na wakati haki ya manabii ilipokuwa imeshindwa; ambapo sheria ilikuwa dhaifu wala haikuweza kuokoa, kwa dhabihu ya mwana-kondoo. Damu ya mnyama na roho ya mnyama haingeweza kurudi. Ilishindwa. Shetani alijua vyema zaidi kuliko hivyo. Ndipo wakati haki ya Mungu, hata hivyo, ikiitisha moto na kuwateketeza wale hamsini, na hukumu ambazo manabii waliitolea nchi, mwanadamu daima aliendelea kwenye upotevu. Kila tumaini lilikuwa limetoweka. Mungu alikuwa ametuma torati, Mungu alikuwa ametuma manabii; na wote walikuwa wameshindwa. Matumaini yote yalitoweka, kwa wanadamu.

¹⁴⁷ Siku moja, katikati ya milki za Utukufu, Mwana wa Mungu akajitokeza. Akasema, “Leo hii, nitakwenda kuwakomboa wana wa Adamu.” Ndipo aliposimama kule ng’ambo, wakati matumaini yote. . .

¹⁴⁸ Ibilisi angeweka magonjwa juu yetu, angeweka dhambi juu yetu, nasi ilitubidi kuichukua; haki ya torati ilidai hilo. Na kama tukishindwa kupokea torati, ambayo sisi sote tumehukumiwa na sheria, haki tu ndiyo itatendeka. Hakukuwa na njia ya kuepukia; hakuna kitu tungeweza kufanya.

¹⁴⁹ Lakini Yeye alijitokeza. Malaika akasema, “Utafanya nini?” Akaenda duniani.

¹⁵⁰ Naye akasema, “Sasa nyinyi, kila mmoja wenu wana wa Adamu, chukueni kile ninachowapa kupigana nacho, na mpigane mwezavyo, vizuri mwezavyo.”

¹⁵¹ Naye kamwe hakupata sehemu dhafu, kupitia theolojia, au wala ujenzi wa seminari, au kujengwa kwa makanisa; bali Yeye alienda mahali ambapo mikuki ilikuwa mizito zaidi, akashuka kupitia bonde la uvuli wa mauti. Naye akakusanya mauti na magonjwa, kwa mikono Yake, akayachomeka kwenye kifua Chake mwenyewe. Kisha akamrudisha Roho Mtakatifu kwenye Siku ya Pentekoste, kumweka mikononi mwetu, na kumwagiza kila mwana wa Adamu kupiga vita kadiri tuwezavyo. Ingawa utadhihakiwa, ingawa utateswa, ingawa utaitwa “mtakatifu anayejibingirisha,” kila kitu kingine; piga vita vizuri uwezavyo, kwa maana ushindi ni wa hakika. Na Mungu ashukuriwe, adui ameshindwa kabisa, ngome zake zimevunjwa, naye Jemadari mkuu wa wokovu wetu anaongoza, leo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹⁵² Ee, wana na binti za Adamu, kwa nini kuketi hapa hapa mpaka mfe? Hebu tuinuke na kufanya jambo fulani. Hebu tuchukue kile tulicho nacho, ikiwa si zaidi ya mdomo wa mwanadamu ambao ungali unaweza kusogea. Na tumpe Mungu sifa. Hebu tumshukuru kwa ajili ya wokovu wetu.

¹⁵³ Ikiwa wewe ni mwenye dhambi, huwezi kamwe kujiita kutoka kwenye machimbo ya dunia hii, ambayo Mungu ameyalipua kwa Injili. Lakini, simama kimya na kumwacha Mungu akukate kwa msumeno, apate kukuweka ndani ya hilo Jengo.

¹⁵⁴ Ikiwa wewe ni mgonjwa, kumbuka, Yesu alishinda mauti, kuzimu, magonjwa, kaburi, na yote, hapo alipokufa kwa ajili yako pale Kalvari. Hebu tuchukue tulicho nacho asubuhi ya leo, na tupige vita kwa ujuzi wetu wote.

¹⁵⁵ Tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi; na kama nikimwomba dada aje acheze piano, wimbo mzuri. Wakati sisi sote. . .

¹⁵⁶ Watu wa busara, wenye akili timamu, je, mnakithamini, asubuhi ya leo, kifo cha Bwana wetu Yesu? Makanisa yenu hayatafaa kitu, ingawaje, kadiri yalivyo mazuri. Shule zenu zitashindwa vibaya, hata hivyo, ingawa ni nzuri kadiri zinavyoweza kuwa. Daktari wako atashindwa vibaya, ingawa ni mzuri kadiri awezavyo kuwa. Lakini, asubuhi ya leo, hebu na tugeuze macho yetu, na tugeuze macho yetu kutoka kwenye sheria za makanisa na madhehebu, na ofisi ya daktari, na kadiri wote walivyo wazuri, na hebu tusikie Sauti hiyo inayotoka kwenye Kivuli kinachotufunika asubuhi ya leo, “Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye.”

¹⁵⁷ Mpendwa Baba wa Mbinguni, kwa unyenyekevu jinsi Wakristo wanavyoweza kukaribia, tunakuja kwa niaba ya waliopotea na wahitaji. Yachukue maneno haya, leo, na, loo, Roho Mtakatifu ambaye analiongoza Kanisa, awafundishe watoto Wako kwa Mungu, leo. Huenda wengi walianguka kando ya njia, wala hawajui njia ya Mungu tena. Wamekuwa giza na wametiwa giza, matumaini yao yameshindwa, lakini wajalie waangalie tena Kalvari, ambapo ulishika mishale yenye moto ya adui wa mauti, adui wa magonjwa, adui wa huzuni, adui wa wanadamu wote. Na hapo ukaichomeka kifua Mwako, na kuifungua njia. Na kupitia kwenye kivuli hicho cheusi, asubuhi ya leo, tunaona Makao yetu Utukufuni.

¹⁵⁸ Kama vile von Winkelried alivyosema, “Nyuma ya ule mlima kuna nyumba, wanangingojea nje, bali hawataniona tena.”

¹⁵⁹ Lakini, Yesu, Wewe hukusema kamwe, “Hawataniona tena.” Ulisema, “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Nitakwenda na kuwaandalia mahali, kisha nje kuwachukua, na kuwapokea Kwangu.” Jinsi tunavyokiheshimu kifo cha ushujaa cha Winkelried; lakini, alikuwa mwanadamu, angeweza tu kufa na kuacha nyuma. Lakini Wewe ulikuja kufa na kukomboa, na kutuleta, si kutoka kwa wapendwa wetu, bali kwa wapendwa wetu; sio kutoka nyumbani mwetu, lakini kutupeleka Nyumbani kwetu. Kisha ukakata mstari kupitia giza la mauti, tupate kuona ng’ambo ya pazia ambako mnakaa baraka za Mungu.

¹⁶⁰ Na sasa, leo, Baba Mpendwa, kama kuna yeyote wa watoto Wako ambaye umemtangazia Injili, kutoka kwenye machimbo ya maisha, na unatamani kuwafanya, na umekuwa ukiwachonga asubuhi ya leo, na kuwakata, ukikatilia mbali tabia zao, na mawazo yao maovu, na masengenyo yao na kurudi nyuma. Na sasa unataka kuwaweka tena, na kuwaingiza kwenye Jengo. Je, utazungumza na mioyo yao sasa hivi?

¹⁶¹ Na tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, kunaweza kukawa na mtoto hapa, leo, ambaye amepotea kutoka kwenye njia, au labda hajawahi kuja kwenye njia? Lakini unajisikia, leo, kwamba ungetaka kujumuishwa; ungetaka kuwa jiwe lililoshikamanishwa kwenye Jengo la Mungu? Naomba umwinulie Kristo mkono wako, useme, “Kristo, katilia mbali mambo yangu ya kilimwengu.”

¹⁶² Mungu akubariki huko nyuma, ewe kijana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, dada yangu. Mungu akubariki. Mtu mwingine?

¹⁶³ Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, tunapomngojea Roho Mtakatifu, nawe unajua kama unamkosea Mungu ama la. Je, ulishindwa kwenda wakati Mshindi wako mkuu aliposema, “Njoo, unifuata. Jitwike msalaba wako, jikane mwenyewe, unifuata. Nitavunja safu za adui. Nitavunja safu za dhambi. Nitavunja safu za maradhi. Na ninyi mnifuata na kupiga vita

vizuri kadiri mwezavyo, kwani nitatoboa tundu ndani yake, na nyumba zetu zitahifadhiwa kwa Uzima wa Milele.”

¹⁶⁴ Je, wewe ni mgeni aliye mbali na Mungu? Inua tu mikono yako, mmoja . . . Mungu akubariki, jamaa mdogo. Mtu mwingine ambaye hajawahi kuinua mikono yao, lakini wakiinua mkono wao. Aseme, “Nikumbuke, Ndugu Branham, leo. Ninataka sasa kuja kwa Kristo. Mimi . . .” Mungu akubariki, dada.

¹⁶⁵ “Ninataka sasa kuja kwa Kristo, kukatwa na mtambo Wake. Kitu fulani asubuhi ya leo kimeugusa moyo wangu. Nimeshtushwa, chini ndani yangu. Nimewekwa kabisa nyuma hapa pamoja na tabia za kidunia, uchafu na matope duniani yamefichua . . . yamenifunika. Lakini Injili, leo hii, imenifichua, nami ninasimama kama mwenye hatia mbele za Mungu, nami ninajua hilo. Na ninataka Mungu anichukue kama jiwe, leo hii, na kunikata, na kunipa ungamo la Bwana Yesu na Roho Mtakatifu, na kuniweka katika Ufalme Wake. Nataka kufichuliwa leo. Ninapofichuliwa, nataka kukatwa kwa msumeno na kuwekwa katika Ufalme Wake.” Je, unaweza kumwinulia mikono yako, kabla hatujafanya maombi kwa ajili ya mwe—mwenye dhambi? Vema.

¹⁶⁶ Kuna mikono minne au mitano ambayo imeinuliwa. Nitawaombea. Sasa hatuna, labda, njia ya kufanya wito wa madhabahuni, labda kama tu utangoja kwa dakika chache tu. Naenda . . . Baada ya kuwaombea wagonjwa, ninawatakeni hapa juu, pia. Lakini nitawaombea sasa, ya kwamba Mungu atawajalia tu jambo fulani maalum wakati huu.

¹⁶⁷ Baba yetu wa Mbinguni, imeandikwa katika Neno Lako Takatifu, kulingana na maandishi ya mwandishi Wako, Mathayo Mtakatifu, mlango wa 5, kifungu cha 24, “Yeye atakayeyasikia Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.”

¹⁶⁸ Sikia ombi nyenyekevu na dhaifu la mtumishi Wako, kwa kila mmoja wa hawa ambao wameinua mikono yao. Ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu.” Nawe umekuwa ukivuta, asubuhi ya leo, nao wamesikia, na wameinua mikono yao. “Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno.” Nami nakushukuru Wewe kwa ajili yao leo. Nami naomba ya kwamba utamtakasa kila mwaminio. Na uwajaze Roho Mtakatifu, wale walio na mioyo yenye njaa, ambayo imeutapika ulimwengu, asubuhi ya leo, nao wanataka kukatwa kama jiwe lililoshikamanishwa kwenye Jengo la Bwana. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

¹⁶⁹ Hivi hamjisikii tofauti kabisa? Hivi Roho Mtakatifu hachukui tu Neno la Mungu kama brashi ya kusugulia, na kusugua tu mambo ya ulimwengu? Kisha unajisikia mpya. Hebu tuimbe wimbo huu mtukufu wa kale, mara nyingine tu tena, kwa

utukufu wa Mungu, sasa. “Kuna Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kutoka kwenye mishipa ya Imanueli.” Wote pamoja sasa. Vema.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
 Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
 Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
 gharika hiyo,
 Hupoteza . . . madoa yao ya hatia.
 Hupoteza madoa yao yote ya hatia,
 Hupoteza madoa yao yote ya hatia;
 Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
 gharika hiyo,
 Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

¹⁷⁰ Nitawaulizeni jambo fulani sasa hivi. Ni wangapi wanaojisikia kuwa dhambi zako zote ziko chini ya Damu? Naomba uinue tu mkono wako. “Sasa ninaamini kwamba Mungu ananisamehe, na mimi—mimi ni mtoto Wake.” Loo, jamani!

Sasa, yule mwizi aliyekuwa akifa, alifurahia
 kuona
 Chemchemi hiyo katika siku yake.

Alikuwa anakufa. Alifurahia kuona Chemchemi hiyo katika siku yake.

Hapo nijalie mimi, ingawa ni mwovu kama
 yeye,
 Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
 zote.

¹⁷¹ Wakati tukiimba kifungu hiki, kisha tuifikie pambio, nataka upeane mikono na mtu anayeketi karibu nawe. Useme, “Mungu akubariki, ndugu Mkristo, dada,” yeyote yule. Sasa, na tumwimbie Bwana sasa. Kwanza, hebu—hebu tuinue mikono yetu, kama tunaweza, na kuimba, “Mwizi anayekufa,” sasa, kwenye pambio, kisha mpeane mikono.

Mwivi anayekufa alifurahia kuona,
 Baba, tunakuabudu Wewe sasa.

. . . Chemchemi katika siku yake;
 Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu
 kama yeye,
 Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
 zote.
 Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
 zote,
 Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu
 zote;

Sasa shikaneni mkono.

Na hapo . . .

Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu zote.

¹⁷² Jinsi tulivyo na furaha leo hii, kama waaminio Wakristo, kama raia wenzi wa Ufalme, kwamba Mungu ameosha na kuondolea mbali dhambi zetu zote, na kutufanya viumbe vipya katika Kristo Yesu! Sasa, je, una furaha kwa ajili ya Bwana? Ajabu!

¹⁷³ Sasa kumbukeni, marafiki, ibada zitarudi hapa tena jioni hii. Mungu awabariki.

¹⁷⁴ Nilichukua muda mrefu zaidi kidogo, asubuhi ya leo, kuliko nilivyokusudia. Nilipata miadi punde tu, baada ya ibada. Kisha nitakutana na baadhi yenu marafiki wapendwa. Sijui kama ingewezekana tungeweza kuahirisha hilo hadi jioni ya leo, nitakaporudi kwenye ibada usiku wa leo. Maana, ninaninii tu . . . Nilidhani ningemaliza kufikia saa tano, na sasa tuna ninii . . . Ni wangapi wa kuombewa? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa, kila mahali. Tuna umati mkubwa wa kuombea.

¹⁷⁵ Nami niliwaaambia jinsi yule Mlutheri, kule juu, alivyoniandikia barua mbaya sana na kunihukumu, na kusema, “Mtu aliyewahubiria watu,” niliowahubiri, “na angesema shetani hawezi kuponya,” na kadhalika. Nami nikamjibu kwa upole tu nijuavyo.

¹⁷⁶ Akajibu tena, barua, na kusema, “Ningependa kukutana nawe kwenye Mkutano wa Wafanyabiashara.”

¹⁷⁷ Nami—nami nikamwuliza Ndugu Moore kama angempa mahali. Akasema, “Naam.”

¹⁷⁸ Nao wakanipeleka nje kwenye seminari ya Kilutheri, na kuandaa mlo wa kutwa kule, ambapo wanafunzi wote na hao walimu. Na huyu alikuwa ndiye mkuu wao; aliketi karibu nami. Ndipo tukala pamoja. Nao walikuwa ni Wajerumani. Na walikuwa na se—se—seti kubwa ya mlo. Nao wa—wanawake wote walituhudumia, na kadhalika. Mlo ulipokwisha, mkuu huyu wa Kilutheri, wa chuo cha Kilutheri, alisimama na kusema, “Ndugu Branham, nilikuleta hapa kwa kusudi moja.” Akasema, “Yaani, tunataka kumpata Mungu katika ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Nikamtazama; nikamwangalia Ndugu Moore. Naye Ndugu Moore akaniangalia. Akasema, “Nilikukosoa, na ninasikitika.” Kasema, “Ndugu Branham, uko sahihi, nami nakuomba unisamehe. Na sasa tunataka ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Akasema, “Tumeona kupigwa mateke kwingi kwa viti na kurarua vitu, lakini,” kasema, “tunamtaka Roho Mtakatifu halisi.”

¹⁷⁹ Nikasema, “Mnaamini?” Akasema . . . Nikasema, “Ni nini seminari ya Kilutheri . . . Ni nini dhehebu la Kilutheri?”

180 Kasema, “Hatulijali dhehebu la Kilutheri. Tunamtaka Kristo.”

181 Na Bob Schuler na hao wengine, mhariri wa Mbiu ya Mkristo, na hao wengine, walikuwa tu wamempokea Roho Mtakatifu, rafiki msiri wa Billy na hao wote. Hao ndugu wana njaa ya Roho Mtakatifu. Ndipo nikasema. . .

Akasema, “Je, ni kwa ajili ya Walutheri?”

Nikasema, “Ni kwa ajili ya, ‘Yeyote atakaye, na aje.’”

Akasema, “Tunawezaje kumpokea?”

Nikasema, “Je, ninyi ni waaminifu kweli?”

182 Akasema, “Naam, Ndugu Branham, kutoka kwenye vilindi vya mioyo yetu.”

Nikasema, “Vipi kuhusu nyinyi wanafunzi?”

183 Kila mkono ukainuliwa, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao. “Tunamtaka Yesu.”

184 Nikasema, “Rudisheni nyuma sahani zenu. Chukueni benchi zenu, mzisukumize pale ukutani.” Kila mtu alifanya hivyo, pande zote. Nikasema, “Sasa pigeni magoti na kuelekeza uso wako ukutani, kisha muanze kumwomba Mungu Roho Mtakatifu.” Nami nikamwomba Ndugu Moore asimame na kuomba. Nikaenda, nikiweka mikono juu ya kila mmoja, basi wanafunzi wote sabini na wawili, pamoja na mshauri wao, wakapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nao wanaitikisa nchi hiyo kule juu, kwa miujiza na matendo ya Mungu. Wana ibada za uponyaji na kila kitu, seminari ya Kilutheri.

185 Loo, ningeweza kuimba niuridhishe moyo wangu! Kwa nini? Unapokuwa na njaa na kiu!

186 Maskini mwanamke huyu, aliyelala hapa, akifa kwa kansa, bila shaka ana njaa na kiu, asubuhi ya leo, Mungu apate kumponya. Na kuna wengi wenu mnaoketi hapo mlio na shida ya moyo. Hakika. Mtakufa mara moja, Mungu asipowaponya. Kuna wengi ambao wana magonjwa mengine, ambayo ni mabaya sana. Lakini, rafiki, usiangalie haki; huwezi kulipa haki. Usiangalie torati, kwa sababu torati haitekelezeki. Lakini, mwangalie Yesu pekee, kwa maana Yeye Ndiye aliyekukombo. Na, kwa imani katika Jina Lake, unaweza kuponywa asubuhi ya leo.

187 Na kama Mungu angewatuma wahudumu sabini wa Kilutheri—Kilutheri, kuihubiri Injili, pamoja na ubatizo wa. . .kwa kuwekewa mikono. Yesu alisema, alipotupatia mambo ya vita vyetu. . .Kama vile von Winkelried, alivyosema, “Tupigane na tulicho nacho.” Haya ndiyo alivyosema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kwa Jina Langu watatoa roho chafu, au pepo. Watanena kwa lugha mpya. Na kama nyoka atawauma, hatawadhuru. Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”

¹⁸⁸ Basi angalieni ule mkato mkuu, kote ulimwenguni sasa, Injili inaendelea. Nao wana wa Adamu, walioitwaa neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, wanapambana wapate njia ya kupitia, na kukata mstari kupitia kwa adui sasa. Na tunachukua kadri tuwezavyo.

¹⁸⁹ Nanyi watu wazima, asubuhi ya leo, mnaothamini afya njema, wakumbukeni hawa tunapowaombea.

¹⁹⁰ Nami nitaomba ya kwamba wagonjwa watapanga mstari upande *huu*, hapa mkono wangu wa kulia. Naomba wazee waje na kuwasaidia, tafadhalini. Pia ninawaomba wahudumu wa Injili, kama watasimama hapa, karibu, na kuomba.

¹⁹¹ Basi msiondoke endapo mnaweza kujizua. Tunataka kufanya wito mwingine wa madhabahuni, kwa muda mfupi tu, haraka tuwezavyo. Ibada hazitamalizika, kwa ibada hii ya uponyaji.

¹⁹² Sasa pageni mstari upande *huu*. Nasi tutamwomba Ndugu Neville, ndugu yetu mpendwa, kama atafanya tunapoendelea kawaida. Kama wanaweza... Mungu akubariki, dada. Ilikuwa ni nini? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu...

¹⁹³ Ungalie upande gani? Kwa Yesu. Madaktari wameshindwa. Kila kitu kingine kimeshindwa. Lakini, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye." Alisema nini? Alisema, "Msikieni Yeye." Alisema nini? Alisema nini?

Amini tu,

Kwa nini? "Mambo yote yanawezekana."

Msilogope, enyi kundi dogo, kutoka msalabani
hadi kwenye Kiti cha Enzi,
Aliingia...uzimani, alikwenda peke Yake;
(...?...)

Yeye...nguvu duniani, nguvu zote Juu,
Amepewa Yeye kwa ajili ya kondoo wa upendo
Wake.

¹⁹⁴ Nguvu zote, kwa ajili ya ugonjwa, kila kitu, amepewa Yeye.

Tu...

Msikieni Yeye. Amini tu!

...-amini,
Mambo yote...

¹⁹⁵ Wakati yote yameshindwa, daktari anaposhindwa, mambo yote yanaposhindwa, Yeye alisema nini? Amini tu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁶ Mia kadhaa, nadhani. Baadhi yao wanakuja katika viti vya magurudumu. Mmoja hapa kwenye machela, akiwa mahututi.

¹⁹⁷ Madaktari wako wapendwa, kama watu wanaoupasua mwili, anatomia, nao wanaangalia na kuona kila kitu wanachoweza, katika maarifa yao, wanajaribu kuokoa maisha, lakini mara nyingi wanashindwa.

¹⁹⁸ Tuna furaha sana kwamba Wingu hili angavu la utukufu lililoning'inia juu Yake, lilisema, "Lakini huyu ni Mwanangu mpendwa." Wakati sheria ilipokuwa imeshindwa, na haki imeshindikana kutimizwa, ndipo Mungu akasema, "Msikieni Yeye." Naye alisema nini? "Mambo yote yanawezekana ikiwa unaweza tu kuamini."

Tusaidie kutokuamini kwetu.

¹⁹⁹ Na kama wahudumu wa Injili, tunaenda sasa kuwapaka mafuta wagonjwa, na kuwawekea mikono, huku watu waliowekwa wakfu wa maskani hii wakiungana pamoja katika maombi. Mungu, bariki juhudi zetu, na uwaponye wagonjwa, tunaomba katika Jina la Yesu.

²⁰⁰ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa katika maombi, na huku kusanyiko likiimba kwa upole *Amini Tu*. Ndugu Neville atapaka mafuta. Nitaweka mikono juu ya wagonjwa.

²⁰¹ Mpendwa Baba wa Mbinguni, sasa hivi kutoka nyuma ya jukwaa, ambapo ninasimama kati ya mauti na uzima, kati ya mwenye dhambi na Hukumu, nikiwaonyesha njia ya kuepukia, ninaitupa nyuma yao sasa na kuweka mikono juu ya mwanamke huyu mgonjwa. Na huku wapendwa wamesimama, wakimtazama, hakuna kitu kimoja kinachoweza kusaidia sasa ila Wewe, ninaweka mikono juu yake, kama Wewe ulivyoagiza...



KUFANYWA WANA WENYE MAMLAKA KIROHO SWA56-0923

(Spiritual Adoption)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 23 Septemba, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org